

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA SITA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA KWANZA

31 JANUARI, 2017

MKUTANO WA SITA
YATOKANAYO NA KIKAO CHA KWANZA – 31 JANUARI, 2017

I. WIMBO WA TAIFA:

Saa 3.00 Asubuhi Wimbo wa Taifa uliimbwa, Mhe. Job Y. Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Bunge.

Makatibu Mezani:

1. Dkt. Thomas Kasilillah
2. Nenelewa Wankanga
3. Charles Mloka
4. Ndg. Neema Msangi
5. Ndg. Joshua Chamwela

II. KIAPO CHA UAMINIFU:

Wabunge wafuatao waliapa Kiapo cha Uaminifu:

1. Mhe. Abdallah Majula Bulembo,
2. Mhe. Anne Kilango Malecela,
3. Mhe. Juma Ali Juma,
4. Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi.

III. TAARIFA YA SPIKA:

Mheshimiwa Spika alitoa taarifa kuhusu Miswada iliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wa Tano wa Bunge na kuwa Sheria. Miswada hiyo ni:-

- a. Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa Mwaka 2016,
- b. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2016.

Aidha, Spika alitoa Taarifa kuhusu Matokeo ya Ushiriki wa Timu ya Bunge kwenye Michezo ya Mabunge ya Nchi za Afrika Mashariki iliyofanyika Mombasa Kenya Tarehe 4 – 10 Desemba, 2016.

IV. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Wabunge na kujibiwa na Mawaziri:-

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 1: Mhe. Omar Abdallah Kigoda
Nyongeza: Mhe. Omar Abdallah Kigoda
Mhe. Ernest David Silinde

Swali Na. 2: Mhe. Juliana Daniel Shonza
Nyongeza: Mhe. Juliana Daniel Shonza
Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu
Mhe. Ester Nicholas Matiko

Swali Na. 3: Mhe. Ester Alexander Mahawe
Nyongeza: Mhe. Ester Alexander Mahawe

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na.4: Mhe. Ally Seif Ungando [Kny Mhe. Muhamed Amour Mohamed]
Nyongeza: Mhe. Ally Saleh Ally

Swali Na.5: Mhe. Dkt. Faustine Englebert Ndugulile
Nyongeza: Mhe. Dkt. Faustine Englebert Ndugulile

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Swali Na. 6: Mhe. Ritta Enespher Kabati
Nyongeza: Mhe. Ritta Enespher Kabati

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Swali Na. 7: Mhe. Moshi Selemani Kakoso
Nyongeza: Mhe. Moshi Selemani Kakoso

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na. 8: Mhe. Salome Wyclife Makamba
Nyongeza: Mhe. Salome Wyclife Makamba

Swali Na. 9: Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu
Nyongeza: Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu

Swali Na. 10: Mhe. Risala Said Kabongo
Nyongeza: Mhe. Risala Said Kabongo

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA
MASHARIKI:**

Swali Na. 11: Mhe. Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala
Nyongeza: Mhe. Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Swali Na. 12: Mhe. Daniel Edward Mtuka
Nyongeza: Mhe. Daniel Edward Mtuka

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Swali Na. 13 : Mhe. Musa Rashid Ntimizi
Nyongeza : Mhe. Musa Rashid Ntimizi

V. MATANGAZO:

- Wageni mbalimbali walikuwepo Bungeni walitambulishwa na Spika kwa pamoja.
- Matangazo ya kazi za Kamati na mengineyo yalitangazwa.
- Spika alitoka Kitini na kumuachia Kiti Naibu Spika.

VI. MWONGOZO WA SPIKA:

Wabunge wafuatao walisimama kuomba Mwongozo kwa Spika:-

1. Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer (Monduli) kwa kutumia Kanuni ya 47 aliomba mwongozo juu ya jambo la dharura kuhusu wananchi wa Loliondo ambao wameamuliwa na Waziri kuondoka katika maeneo yao na pia mifugo yao kutaifishwa na kwamba jambo hilo linaleta mgogoro mkubwa kati ya wakulima na wafugaji. Aliomba Bunge liielekeze Serikali kutekeleza jambo hilo kwa kuzingatia Maamuzi yaliyokwishafanyika awali.

Naibu Spika alitoa uamuzi kuwa Mbunge atumie Kanuni nyingine kuleta suala hilo Bungeni ili lijadiliwe kwa kuwa siyo jambo la dharura.

2. Mhe. John Wegesa Heche (Tarime Vijijini) alitumia Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo kuhusu wananchi wa Kagera kuathirika na Mvua na nyumba zao kubomolewa na Tetemeko la Ardhi. Aliomba michango ya Wabunge waliyochangia kwa ajili ya Wahanga irejeshwe ili iwasaidie wananchi hao.

Naibu spika alitoa uamuzi kuwa kiti hakina taarifa za kutosha kuhusu athari za Mvua Mkoani Kagera.

VII. HOJA YA KUTENGUA KANUNI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu alitoa Hoja ya kutengua Kanuni zifuatazo:-

- a. Kanuni ya 28(2) ili Bunge lirejee saa 10.00 jioni badala ya saa 11. 00 jioni kuanzia tarehe 3 Januari, 2017.
- b. Kanuni ya 62(15) ili Bunge likutane siku ya Jumamosi tarehe 4.2. 2017.
- c. Kanuni ya 62(1)(a) ili muda wa wachangiaji uwe dakika 10 badala ya dakika 15.

Hoja hii iliungwa mkono na kukubaliwa na Bunge baada ya kuhojiwa.

VIII. KAULI ZA MAWAZIRI:

Kauli zifuatazo zilitolewa na Mawaziri:-

- a. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi alitoa kauli kuhusu Hali ya Chakula Nchini; na
- b. Waziri wa Fedha na Uchumi alitoa Kauli kuhusu Deni la Taifa na Hali ya Uchumi Nchini.

IX. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wa Mwaka, 2016 (*The Legal Aid Bill, 2016*).

- a. Waziri wa Katiba na Sheria alitoa Maelezo ya Muswada na kutoa Hoja ya kuliomba Bunge Ijadili na kuupitisha.
- b. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria alisoma Taarifa ya Kamati kuhusu Muswada huo.
- c. Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu, Msemaji Mkuu wa Kambi Upinzani Bungeni wa Wizara ya Katiba na Sheria alitoa maoni ya Upinzani kuhusu Muswada huu.

Michango ya jumla ilianza kwa Wabunge wafuatao kuchangia:-

1. Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa – CCM
2. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab – CCM

X. KUSITISHA BUNGE:

Saa 7.00 mchana Naibu Spika alisitisha Bunge hadi saa 11.00 jioni. Aidha, Wabunge walikataa hoja ya kuongeza muda wa dakika 30 ili wachangiaji watatu wachangie mchana huo.

XI. BUNGE KUREJEA:

Bunge lilirejea saa 11.00 jioni na kuongozwa na Naibu Spika, mjadala wa Muswada uliendelea kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Taska Restituta Mbogo – CCM
2. Mhe. Ally Saleh Ally – CUF
3. Mhe. Selemani Jumanne Zedi - CCM

XII. KUHITIMISHA MUSWADA:

Waziri wa Katiba na Sheria alipewa nafasi ya kuhitimisha Muswada na kujibu Hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge.

XIII. KAMATI YA BUNGE ZIMA:

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Bunge Zima ili kupitisha Muswada Ibara kwa Ibara. Ibara ya 14 ilipitishwa pamoja na marekebisho ya Mhe. Ruth

Hiyob Mollel kama alivyoishauri Serikali. Baada ya hapo Kamati ya Bunge Zima ilipitia ibara zote 49 pamoja na marekebisho yake na kuyapitisha.

XIV. BUNGE KURUDIA.

Bunge lilirudia na mtoa Hoja alitoa taarifa ya kazi ya Kamati na kutoa Hoja kuwa Bunge likubali kupitisha Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wa mwaka 2016. Hoja iliungwa mkono, Bunge lilihojiwa na kupitisha Muswada.

TANGAZO: Naibu Spika alitoa majibu ya Mwongozo uliombwa asubuhi kuhusu muda wa kuwasilisha marekebisho (*amendments*) ya Miswada.

XV. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 12.45 jioni, Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano tarehe 1/2/2017 saa 3.00 asubuhi.

DODOMA

31 JANUARI, 2017

DKT. T. D. KASHILILAH

KATIBU WA BUNGE